SCHOOL BASED ASSESSMENT SHUGHULI ZA KISWAHILI - GRADE 3 EXAMS TERM 1 2023

Maswali

SEHEMU YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

1. Mwanafunzi anapewa shuleni akisoma, yeye huwa anafurahia haki gani?
2. Mtoto anapopewa chakula bora na mzazi wake, yeye hupata haki gani?
3. Mtoto akiwa mgonjwa anafaa kusaidiwaje?
4. Haki ya kucheza hupatikanaje?
5. Ni kwa nini watoto hawafai kuvalia nguo zilizoraruka?

SEHEMU YA 2: KUSOMA
Zoezi la 1: Kusoma kwa sauti.
Soma hadithi hii kwa sauti.
Samira ni mvuvi katika kijiji cha Saragambo. Yeye hupenda kuvua wakati wa asubuhi. Samaki hao yeye huwauza katika soko la Uyoma. Anao watoto watatu ambao anawapenda sana. Samira ana bidii sana. Watu wa kijiji chake humpenda sana Samira.
Alama 10

Zoezi la 2: Kusoma kwa ufahamu
Soma hadithi hii na ujibu maswali
Jumamosi iliyopita, shangazi yangu alitutembelea. Hakuwa ametutembelea kwa muda wa wiki mbili. Alinileta peremende na biskuti. Baba na mama walifurahi sana kwa kumwona. Hata hivyo, nilikuwa na furaha kuliko wao. Siku iliyofuata, Jumapili, mimi na shangazi tulienda kanisani ambapo tuliimba na kumchezea Mungu. Ilikuwa ni siku njema.

11. Shangazi wa mwandishi aliwatembelea siku ya .....
12. Shangazi wa mwandishi alimietea mwandishi.....
13. Mwandishi alienda kanisani pamoja na.....
14. Kina mwandishi walienda kanisani siku ya.....
15. Walipokuwa kanisani, waliimba na kumchezea.....

SEHEMU YA 3: SARUFI
Chagua jibu sahihi kutoka mabanani.

16. Wavulana.....liokuja wapewe viti (tu, ni, va).
17. Sisi sote.....tapewa zawadi (ni, wa, tu).
18. Yeye.....pendi kunywa maziwa (si, hu, ha)

Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.